# Learning by Ear 2009
# Children's Rights Series
# 05 The right to physical integrity

**Subject**: Violence and abuse, the right to physical integrity

**Author**: Valérie Hirsch (South Africa)

**Editor**: Sandrine Blanchard

**Translation**: Anne Thomas

**Kisuaheli** **Eric Ponda**

| | Women | Men | Age | |
|---|---|---|---|---|
| IN/OUTRO | X | | Unimportant | |
| Narrator | | X | Ca. 25 | |
| Yolanda | X | | 16 | English |
| Pastor Schroeder | | X | 28 | English |
| Engelo (Yolanda's mother) | X | | adult | English |

| LbE soundtrack |
|---|

**INTRO:**

Hujambo msikilizaji mahali popote ulipo na karibu kwa makala ya tano kwenye mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga Maisha yako. Tukiwa bado tunazungumzia masuala ya haki za watoto na juhudi za kudumisha amani. Leo tunafunga safari hadi nchini Afrika Kusini ambako tunakutana na Yolanda, msichana aliyewahi kubakwa mara mbili. Na kila wakati alipobakwa, Yolanda alikuwa akilaumiwa kuwa chanzo cha uovu huo. Sikiliza kwa makini.

**Musical interlude**

**Narrator:**

Yolanda Combrick ni raia wa Afrika Kusini. Ana umri wa miaka 16 na mrembo. Yeye ni mzungumzaji na mcheshi sana. Asilia yake ni mchanganyiko wa Mwafrika na Mzungu anayeishi katika kitongoji cha watu wanaoishi maisha ya kadri mjini Johannesburg.

Mnamo mwezi Machi mwaka 2008 Yolanda alibakwa na mjombake mwenye umri wa miaka 64, aliyemvamia bafuni.

**1. Yolanda assault uncle 1’06’’ (English)**

Usiku huyo wa Jumamosi, tulikuwa tumeandaa karamu ya familia, binamu yangu alikuja na kuniambia mjomba alitaka kunibusu. Nilichukulia jambo la mzaha tu na sikumuamini binamu yangu. Lakini siku iliyofuatia

niliamini kwani mjomba alinisimamisha na kuanza kunipapasa matiti huku akijaribu kunivua nguo na kupeleka mkono wake hadi sehemu zangu …….. za siri . Nilimwambia tafadhali usifanye hivyo!”. Kwa bahati nzuri mama aliniita na hapo akaniachilia. Nilijiuliza maswali mengi kwa nini mjombangu afanye hivi, na huku nikijilaumu kwa kushindwa kujitetea. Kisha nikapiga moyo konde nakusema si makosa yangu!

**Narrator:**

Yolanda hakumwambia mtu yoyote kuhusu yaliyotokea isipokuwa binamu yake. Alimuogopa sana mjombake na hakujua familia yake angechukuliwa vipi suala hilo.

Lakini kwa kuwa mwanzo wa ngoma ni lele. Kisa kilichofuatia kilimfanya kuzungumzia hadharini uovu huo. Mnamo January mosi mwaka 2009, Yolanda akiwa likizoni alienda matembezi na familia yake katika sehemu walipopiga kambi. Yolanda alikuwa amefanya urafiki na watu wengi akiwemo mvulana mmoja wa umri wa miaka 19. Siku moja mvulana huyu alimtaka Yolanda kimapenzi na kumuuliza kulala naye, lakini akakataa. Siku iliyofuatia, wakiwa wanaogelea na rafiki zake kwenye kidingwi, alitoka kwenda kujisaidia chooni ambako mvulana huyu alimufuata akitaka kuzungumza naye. Yolanda akamwambia amsubiri mlangoni:

**2. Yolanda rape narrative – 56’ (English)**

Nikiwa bafuni, alisukuma mlango kutaka kuingia kwa nguvu. Nilipojaribu kuzuia mlango aliingia na kunibaka. Kisha baada ya kumaliza shughuli

zake akaniuliza “je umefurahia ?” na kama ilivyo kawaida kwa wasichana kumwambia “ ndio nimefurahia” Nilisema hivyo kwa sababu niliogopa angenipiga, sikujua la kufanya, hivyo nikamwambia “ndio nimefurahia!”Baadaye aliniambia kwamba atamwambia kwa kila mmoja kambini kwamba nilikubali kufanya naye mapenzi hivyo hayakuwa makosa yake. Niliudhika, nilihuzunika, niliogopa zaidi. Wakati mwengine hujiuliza kwa nini mambo haya yalinipata mimi?” Nilijilaumu lakini kisha nikapiga moyo konde kwamba halikuwa kosa langu.

**3. Atmo church**

**Narrator**

Ilimchukua Yolanda muda wa wiki moja kumweleza mchungaji wake kuhusu yote yaliyotokea. Hatimaye alikuwa amepata faraja. Tangu siku hiyo Yolanda alikuwa akimtembelea mwanasaikolojia kanisani na kituo cha kupambana na unyanyasaji wa kimapnezi kila wiki kupata ushauri wa kitalaam.

Kutokana na msaada huo, Yolanda alipata ujasiri wa kumweleza mamake pia kuhusu yaliyotokea. Lakini mamake hakumuamini:

**4. Yolanda « mum's reaction » (English)**

Mamangu hataki kuelewa. Hakuamini kwamba mjombangu angeweza kunitendea unyama huo, akisema kuwa mimi ndiye niliemshawishi kijana huyo kunibaka. Lakini la hasha! Nilikuwa mtu na fahamu zangu na

nilitaka sana kuhifadhi hadhi yangu, lakini pia nilitaka kuwa rafiki kwa kila mmoja. mamangu hakuniamini kabisa. Natumai urafiki baina ya mimi na mamangu utazidi kudumu ingawa najua haitakuwa rahisi. Mara nyingi Mamangu ameniambia ananipenda lakini babangu hata siku moja! Nafikiri hii ndio sababu nilitaka sana urafiki na wavulana. Nilitaka kupendwa namna hiyo.

**5. Atmo Yolanda+mother**

**Narrator**

Mamake Yolanda,Engelo Combrick, ni mtu mwenye kutaka kudumisha uelewano katika familia yake. Na ndio maana alionelea kuweka siri yote yaliyompata binti yake ili asivuruge amani katika familia hiyo. Hakumuamini Yolanda na hata kumwita muongo.

**6. Engelo- mother (English)**

Nilishtuka sana niliposikia habari hizo za mjombake, ni jambo la kushangaza sana. Sikuamini kabisa. Na nikamwambia binti yangu hata kama ni kweli, afyate mdomo wake. Hata mume wangu alikuwa hajasikia habari hizo. Wazazi wangu pia hawakuwa na habari. Na nina wasiwasi wakati watakapojua ukweli wa mambo. Sikujua la kufanya kuhusu suala hili, lakini lililokuwa dhahiri ni kwamba ndoa yangu pia ilikuwa imo hatarini, kwa sababu tumemsaidia sana mjomba, kwa chakula, mavazi, kimsingi kwa kila kitu, na sielewi ni kwa nini angeweza kumtendea

unyama binti yangu. Mume wangu ni mkali sana, na anaweza hata kuniua akisikia habari hizi. Naogopa sana kama jambo hili litafichuka. Hata wazazi wangu, shemeji wangu wote. Kutazuk ala kuzuka, mambo yatakuw amagumu sana

**7. Turn up Atmo Yolanda+mother**

**Narrator**

Yolanda pia ana hofu jinsi atakavyochukuliwa na familia ya mamake. Lakini ushauri aliopata umemshawishi kwamba ana haki ya ili kuwakinga wasichana wengine wasipitie uovu kama huo. Waathiriwa wa ubakaji kawaida huwa na kiwewe. Hisia hotofuatiana lakini madaktari wametambua awamu tatu baada ya hujuma kufanyika. Kwanza kabisa, ni mshtuko, awamu ambapo hofu kutawala. Pili ni kujipanga upya ambapo muathiriwa polepole hufanya shughuli zake za kila siku. Na mwisho ni maingiliano ambayo yanaweza kuchukua muda mrefu. Hii ni awamu ambapo muathirika polepole hupata utulivu wa kisaikolojia na kurejea katika maisha ya kijamii.

**8. Yolanda family reaction (English)**

Sasa naweza kulizungumzia suala hilo wazi wazi, lakini miezi michache iliyopita singeweza kabisa.Ingawa bado nina uoga kidogo kulizungumzia, nataka kuliweka wazi kwamba watu hawa ni hatari. Naelewa kwamba familia yangu itanikasirikia sana kiasi cha kunitenga kwa jinsi wanavyomchukulia mjombangu. Familia yangu ingekasirika sana na hata

kunitenga. Kama nilivyotangulia kusema sinahaja ya kujilaumu mwenyewe. Si kos alangu lakini najua watamuamini zaidi mjombangu kwa sabanu mimi bado ni mototo na yeye ni mtu mzima.

**9. Atmo Yolanda+pastor**

**Narrator**

Yolanda amestahamilia machungu yote aliyopita hasa kutokana na usaidizi na ushauri wa mchungaji Werner Schoeder. Kasisi huyu mwenye umri wa miaka 28 pia anaonekana kijana na labda ndio sababu aliweza kurejesha imani ya msichana huyu. Amekuwa mshauri wake mkubwa tangu alipokumbana na masaibu hayo. Anafahamu kwamba wakati mtoto anapobakwa kawaida wazazi huwa wa mwisho kufahamishwa. Sasa ni miezi miwili tangu kisa hicho kitokee na Yolanda hajamweleza Babake:

**10. Pasteur Werner Schroeder –1'21'' (anglais)**

Aliogopa kuelezea familia yake. Na mtu pekee aliyemuelezea ni mpwawe kanisani..Nafurahi tuko hapa. Nasikitika pia kuwa imechukua muda mrefu. Si haki kukabiliana na donda hili moyoni kwa muda mrefu, hususan kama msaada unapatikana. Naweza kusema kuwa kumekuwa na mabadiliko makubwa tangu tulipoanza kumsaidia hadi wakati huu. Hata hivyo bado kuna kazi kubwa ya kufanya kurejesha imani yake ili aweze kurejelea maisha yake ya kawaida na kuendelea kutangamana na marafiki. Nafikiri Yolanda bado anahitaji muda zaidi kuweza kuwaamini tena watu anaotangamana nao. Ni msichana mpole na pia mchangamfu.

Maisha yake yameathiriwa na kijana aliyemdhania kuwa rafiki tu ambaye alitumia fursa hiyo kumtendea ukatili. Yeye huwavutia wavulana kwa urahisi na haraka kutokana na urembo wake, lakini kwa niaba yake nimewahi kuwashauri vijana waliomtaka kimapenzi na kukataliwa. Naamini mshauri wake ataendelea na juhudi za kumfunza kujikinga au kujiepusha na maovu , kama vile kuwa na urafiki wa karibu au kuwaamini kwa urahisi watu asiowafahamu vyema.

**11. Atmo church**

**Narrator**

Mwanzoni mwa mwaka mshauri huyu aliweza kumshawishi Mamake Yolanda kwamba aliyokuwa akizungumza binti yake ni ya kweli. Kisha Yolanda akaenda hadi kituo cha polisi kuripoti visa hivyo viwili, cha Babake mdogo na pia mvulana aliyembaka bafuni. Hata hivyo haitakuwa rahisi kusahau yote yaliyompata ingawa amepata nguvu mpya za kukabiliana na hali hiyo ya kunyanyaswa kimapenzi

**Atmo singing in church**

**OUTRO:**

Ripoti hii iliyoandika na Valérie Hirsch kutoka nchini Africa Kusini ndipo tunapokamilisha makala yetu ya leo Learning by Ear Noa bongo jenga maisha yako.Ukipenda kusikiliza tena makala haya na vipindi vingine vinavyotayarishwa na Deutsche Welle usikose kutembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine tutakapokutana tena kwa makala nyingine kwaheri kwa sasa.

| **End music** |
|---|